**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**

***(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke)***

**Kumb. Na.** TMC/MD/B.2/37/118 **Tarehe:** 09/03/2026

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Manispaa ya Temeke kuomba nafasi ya kazi zilizotajwa hapo chini.

### 1.0 AFISA MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA II - NAFASI (10)

**(a) SIFA ZA KUAJIRIWA**

Awe mwenye Stashahada **(Diploma)** ya Uuguzi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga.

Kazi na majukumu

i) Huduma za uuguzi
ii) Kukusanya takwimu muhimu za afya.
iii) Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yako
iv) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao kiafya
v) Kutoa huduma za kinga na uzazi
vi) Kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na mkuu wako wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wako.

### 2.0 MHUDUMU WA AFYA - NAFASI (21)

92 Barabaraya Mandela / Taifa, S.L.P 46343, Dar es Salaam, Simu +255222928132, Nukushi +255222928137,
BaruaPepe: temeke@temekemc.go.tz , Tovuti: www.temekemc.go.tz

CS CamScanner

### (a) SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe amehitimu kidato cha nne na kupata mafunzo ya mwaka mmoja katika fani ya afya.

Kazi na majukumu

i) Kufanya usafi wa vifaa vya kazi, usafi wa wodi na mazingira
ii) Kusaidia wagonjwa wenye ulemavu na wasiojiweza katika kwenda haja (kubwa na ndogo) na kuoga
iii) Kumsaidia kumlisha mgonjwa asiyejiweza
iv) Kuchukua nguo za mgonjwa kuzipeleka kwenda kufuliwa
v) Kuchukua sampuli za mgonjwa kwa ajili ya vipimo vya maabara na kufuatilia majibu.
vi) Kutayarisha vifaa kwa ajili ya kusafisha na kufunga majeraha
vii) Kufuatilia mahitaji ya dawa kwa wagonjwa kutoka hifadhi ya dawa
viii) Kufanya shughuli nyingine utakazopangiwa na kiongozi wako wa kazi.

## 3.0 MTEKNOLOJIA MIONZI - NAFASI (02)

### (a) SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe mwenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika

Kazi na majukumu

i) Kutibu wagonjwa wanaoelekezwa kwenye eneo lako la kazi kwa mionzi sahihi iliyoelekezwa na Daktari Bingwa wa Mionzi
ii) Kutunza miambo na vifaa vya Radiotherapia katika eneo lako la kazi
iii) Kukagua na kusimamia ubora wa mionzi inayotolewa na mitambo ya Radiotherapia (Radio – therapeutic quality)
iv) Kusimamia watumishi walio chini yako
v) Kutoa ushauri kuhusu masuala ya kazi ya Radiotherepia na mionzi katika eneo lako la kazi.

92 Barabaraya Mandela / Taifa, S.L.P 46343, Dar es Salaam, Simu +255222928132, Nukushi +255222928137,
BaruaPepe: temeke@temekemc.go.tz , Tovuti: www.temekemc.go.tz

CamScanner

vi) Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji wa vifaa katika eneo lako la kazi (sterilization)

vii) Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lako la kazi.

viii) Kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na mkuu wako wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wako.

## 4.0 MTEKNOLOJIA DAWA - NAFASI (06)

### (a) SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe mwenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika

Kazi na majukumu

i) Kuainisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lako la kazi.

ii) Kugawa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na watumishi

iii) Kuchanganya dawa

iv) Kuhifadhi dawa na vifaa tiba

v) Kukagua dawa, vifaa tiba, kemikali, vitendanishi na vipodozi katika eneo lako la kazi

vi) Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa

vii) Kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa

viii) Kuratibu kazi za kamati ya dawa za Hospitali

ix) Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba

x) Kufanya uchunguzi wa ubora wa dawa, vifaa tiba, kemikali, vitendanishi na vipodozi.

xi) Kufanya kaguzi mbalimbali katika sehemu zinazohifadhi dawa

xii) Kusimamia utendaji wa kazi za watumishi walio chini yako

xiii) Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba.



CamScanner

xiv) Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lako la kazi

xv) Kufanya kazi nyingine utakazopewa na mkuu wako wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wako.

## 5.0 MUUGUZI II - NAFASI (34)

### (a) SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe mwenye Stashahada (Diploma) ya uuguzi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

Kazi na majukumu

i) Huduma za uuguzi
ii) Kukusanya takwimu muhimu za afya
iii) Uwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
iv) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
v) Kutoa huduma za kinga na uzazi
vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi zinahusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

## 6.0 TABIBU - NAFASI (02)

### (a) SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe mhitimu wa Kidato cha Nne/sita mwenye Stashahada **(Diploma)** ya Tabibu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

Kazi na majukumu

i) Kazi zote zinazofanywa na Tabibu Msaidizi
ii) Kutambua na kutibu magonjwa ya kawaida
iii) Kusimamia utendaji wa Watumishi walio chini yake na kufanya upasuaji mdogo
iv) Kushiriki katika kupanga na kutekeleza huduma za Afya Msingi



CamScanner

v) Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia Huduma za Afya za Mfuko wa jamii
vi) Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma
vii) Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji
viii)Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi
ix) Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za Afya za Mfuko wa Afya ya Jamii

## 7.0 TABIBU ANASTEZIA - NAFASI (03)

### (a) SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe mhitimu wa Kidato cha Nne/sita mwenye Stashahada **(Diploma)** ya Tabibu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali,

Kazi na majukumu

i) Kutathimini utayari wa wagonjwa kabla ya upasuaji
ii) Kuanzisha ganzi katika chumba cha Upasuaji
iii) Kufuatilia wagonjwa wakati wa taratibu wa matibabu
iv) Kurejesha ganzi na kudhibiti maumivu baada ya upasuaji
v) Kufanya kazi za usimamizi wa matibabu
vi) Kufunza na kusimamia wafanyakazi wadogo

## 8.0 MHASIBU – NAFASI (01)

### (a) SIFA ZA KUAJIRIWA

Kuajiriwa wenye mojawapo ya sifa zilizotajwa hapo chini: -

1. Intermediate certificate inayotolewa na NBAA
2. Shahada ya Biashara/Sanaa yenye mwelekeo wa Uhasibu au Stashahada ya juu ya Uhasibu kutoka Chuo Kikuu/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali
3. Stashahada ya juu ya Uhasibu Serikalini (Advanced Diploma in Government Accounting) inayotolewa na Chuo cha Uhasibu Dar es Salaam.

92 Barabaraya Mandela / Taifa, S.L.P 46343, Dar es Salaam, Simu +255222928132, Nukushi +255222928137, BaruaPepe: temeke@temekemc.go.tz , Tovuti: www.temekemc.go.tz

CS CamScanner

4. Na wenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu katika fani ya Uhasibu.

Kazi na majukumu

i) Kuidhinisha hati za malipo
ii) Kuandika taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi
iii) Kusimamia Wahasibu wasaidizi katika kazi zao za kila siku
iv) Kusimamia shughuli za uhasibu kwenye kitengo cha Idara
v) Kuandika taarifa ya maduhuli
vi) Kufanya kazi za kiuguzi na kuhudumia wateja katika jamii na hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.

**9.0 AFISA MUUGUZI II - NAFASI (06)**

**(a) SIFA ZA KUAJIRIWA**

Awe mwenye Shahada ya Uuguzi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliohitimu mafunzo ya vitendo kazini **(Internship)** na waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

Kazi na majukumu

i) Kufanya kazi za kiuguzi na kuhudumia wateja katika jamii na hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za Afya
ii) Kukusanya takwimu muhimu za Afya
iii) Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
iv) Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani
v) Kutoa Ushauri nasaha
vi) Kutayarisha mpango wa kazi kwa ajili ya huduma za uuguzi
vii) Kuelimisha wagonjwa na jamii
viii)Kutoa huduma za kinga na uzazi
ix) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.



CamScanner

## 10 MFAMASIA - NAFASI (02)

### (a) SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe mwenye Shahada ya Famasi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, aliyehitimu mafunzo ya vitendo kazini **(Internship)** ya mwaka mmoja ambao wamesajiliwa na Baraza la Famasi.

Kazi na majukumu

i) Kuanisha mahitaji ya mwaka ya dawa na vifaa na kuandaa bajeti yake
ii) Kuagiza, kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa na vifaa tiba katika kituo chake cha kazi
iii) Kuweka kumbukumbu za dawa
iv) Kutoa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa
v) Kuandaa orodha ya dawa za hospitali (Hospital Fomulary) kwa matumizi ya kituo anapofanya kazi
vi) Kusimamia matumizi sahihi ya dawa
vii) Kukagua maduka ya dawa katika sekta binafsi
viii) Kutengeneza dawa **(compounding)** kwa matumizi ya kituo anapofanyia kazi
ix) Kutoa taarifa juu ya madhara yanayotokanayo na matumizi ya dawa (adverse drug reaction)
x) Kuwa Katibu wa Kamati za Tiba ya Hospitali **(Hospital Theraputic Committee)** anapofanya kazi
xi) Kuelimisha Watumishi waliochini yake, watumishi wengine wa sekta ya Afya na jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa
xii) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Dawa katika kituo anapofanya kazi
xiii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

## 11 MTEKNOLOJIA MAABARA - NAFASI (09)

### (a) SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe mwenye Stashahada katika Fani ya Uteknolojia katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali,na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.



CamScanner

Kazi na majukumu

i) Kupima sampuli zinazotolewa maabara
ii) Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekewa maabara ngazi za juu
iii) Kufanya kazi za ukaguzi wa maabara, vitendanishi, vifaa,kemikali na hifadhi ya kemikali
iv) Kuweka kumbukizi za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi
v) Kufundisha watumishi walio chini yake
vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**MASHARTI KWA UJUMLA KWA WAOMBAJI**

I. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
II. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
III. Waombaji ambao tayari ni Waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na**. CCA.45/257/01/D/140** wa tarehe **30 Novemba, 2010**.
IV. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza **(Details CV)** anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini **(Referees)** watatu wa kuaminika.
V. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha Nne, Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
VI. Testmonials Provisional Results Statement of Results hati matokeo ya kidato cha nne na sita **(FORM IV, FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**



CamScanner

VII. Waombaji walisoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika **(TCU, NECTA na NACTE)**

VIII. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

IX. Waombaji wenye majina tofauti katika vyeti vya Taaluma, Kuzaliwa na NIDA waambatishe **DEED POLL (Hati ya usajili wa kiapo cha Majina)**

X. Waombaji ambao wanautofauti wa Herufi katika kitambulisho cha Taifa na Vyeti vya Taaluma, Kidato cha Sita, Kidato cha Nne na cha Kuzaliwa wanatakiwa kuambatisha **AFFIRDAVIT (Kiapo)**

XI. Waombaji wote ambao kazi zao zinahitaji leseni waambatishe nakala za leseni.

XII. Waombaji watakao wasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria.

**MUHIMU:**

Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **20/03/2026** saa 9:30 alasiri

Anwani ya kutuma

**Mkurugenzi Manispaa**
**Halmashauri ya Manispaa ya Temeke**
**S.L. P 46343**
**DAR ES SALAAM**

**Imetolewa na:**

Jomaary Satura
**MKURUGENZI**
**MANISPAA YA TEMEKE**



CamScanner